# CHUO CHA UFUNDI STADI TURNBULL MKOANI IRINGA

# SIKU YA TURNBULL (TTTC), 02/10/2026

# MIAKA 9 YA MAFUNZO.

# TAMBALA NG'OMBE HOSPITAL SADANI –MAFINGA

Chuo cha ufundi stadi Turnbull (TTTC) ni chuo kinachotoa mafunzo ya aina mbalimbali hapa mkoani Iringa na vilevile ni chuo ambacho kimesajiliwa na Serikali kwa usajili wa REG/NACTVET/1320. Pamoja na kutoa mafunzo ya fani mbalimbali chuo cha Turnbull mwaka 2023 kilianzisha mpango mkakati maalum wa kila mwaka siku ya Turnbull Tech College kuwa na matendo ya huruma ya kugusa makundi maalum ndani ya jamii yetu kama vile:-

1) Walemavu
2) Wagonjwa Hospitalini ✓
3) Watoto Yatima na wenye mazingira magumu
4) Wajane na Wazee
5) Kutembelea Wafungwa Magerezani

Kwa muktadha huo basi, kwa kuendeleza mpango mkakati wetu wa kugusa makundi hayo chuo cha Turnbull mwaka huu 2026 kimejiwekea mkakati wa kutembelea **TAMBALA NG'OMBE HOSPITAL SADANI** tarehe 02/10/2026 kwa neema ya Mungu.

Matendo yetu ya huruma kwa mwaka huu yatafanyika katika hospital ya TAMBALA NG'OMBE iliyopo Sadani, kwa ushirikiano mkubwa wa wadau mbalimbali. Hivyo basi tunategemea kufanya matendo ya huruma kwa kutoa vitu vifuatavyo kadri Mungu atakavyotuwezesha kuvipata kutoka kwa Wadau wetu:

**VITU TUNAVYOTEGEMEA KUTOA KWA WAGONJWA NI KAMA IFUATAVYO:-**

| ***S/No:*** | ***ITEMS*** | ***S/No:*** | ***ITEMS*** |
|---|---|---|---|
| ***1.*** | *NGUO* | ***9.*** | *SABUNI ZA MCHE* |
| ***2.*** | *CHUMVI NA SUKARI* | ***10.*** | *SABUNI ZA UNGA & ZA MAJI (Chooni & za kawaida)* |
| ***3.*** | *GROVES* | ***11.*** | *DAWA ZA MENO NA MISWAKI* |
| ***4.*** | *UNGA WA LISHE* | ***12.*** | *VIFAA VYA USAFI (Mifagio, Ndoo, Leki nk.)* |
| ***5.*** | *VIATU* | ***13.*** | *NETI (Vyandalua) na dawa ya kuulia wadudu* |
| ***6.*** | *TAULO ZA KIKE (PEDI)* | ***14.*** | *MAJI, MAZIWA, PAMPASI & WAPS* |
| ***7.*** | *MAFUTA YA KULA & YA KUPAKAA* | ***15.*** | *VITABU VYA IMANI NA VITABU VYA KUELIMISHA* |
| ***8.*** | *MAJANI YA CHAI* | ***16.*** | *MAHARAGWE, BLUE BAND & PEANUT BUTTER* |

**LENGO LA TUKIO HILI NI KAMA IFUATAVYO:**

{1} Kutoa **Faraja, Upendo na Msaada**
{2} Kutoa msaada wa Kiroho kwa wagonjwa ili kuwapa tumaini jipya kutokana na changamoto wanazopitia za kiafya.
{3} Kukuza moyo wa huruma na kujitoa kwa wanafunzi wetu, wadau wetu na jamii kwa ujumla
{4} Kujenga mahusiano mazuri kati ya Chuo na Jamii kwa kushirikiana katika kusaidia wenye uhitaji.

Tunatambua kuwa hatuwezi kufanikisha jambo hili pasipo msaada wa wadau na watu wenye moyo wa huruma kama wewe. Kwa heshima na taadhima, tunakuomba kushiriki nasi kwa namna yoyote ile utakavyoona inafaa, iwe ni kupitia msaada wa vitu tajwa hapo juu, fedha, au hata ushauri na uwepo wako wakati wa ziara yetu.

***TAREHE YA ZIARA:*** **02/10/2026 –**Gharama za usafiri kwenda na kurudi zitatoka ofisini.

**MAHALI:** Hospitali ya **TAMBALA NG'OMBE**, Sadani -Mkoani Iringa.

Tunaamini kuwa kwa pamoja tunaweza kuleta tabasamu, faraja na Upendo kwa wale walioko hospitalini, tukiwakumbusha kuwa bado wanapendwa na kuthaminiwa na jamii.

***"Upendo wa kweli ni kuwagusa wengine kwa namna ya tofauti"***

Tunatanguliza shukrani zetu za dhati kwa moyo wako wa upendo na msaada.

Barua pepe (E-Mail Address): info@turnbullcollege.ac.tz
Tovuti (Website) www.turnbullcollege.ac.tz

**MAWASILIANO: 0623561873 AU 0622298845 AU 0734305992**

***KESHO YETU HATUIJUI!!***
***HIVYO***
***TTTC - TUNAWAKARIBISHA SANA MATENDO HAYA YA HURUMA KWA WAGONJWA.***